




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb. Na. NDC/I.20/6/VOL.VII/179

3/08/2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anawatangazia nafasi 1 ya kazi na anakaribisha maombi kwa watazania wote wenye sifa na uwezo, kwa ajili ya kujaza nafasi ya kazi kama ilivyo orodheshwa katika tangazo hili. Aidha mnajulishwa kuwa mwisho wa maombi haya ni tarehe 16/8/2023.

1.MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – NGAZI YA MSHAHARA TGS C (NAFASI 1)

a) Sifa za mwombaji.

Waombaji wawe wamehitimu kidato cha nne au sita wenye Stashahada au NTA Level 6 katika Fani ya Utunzaji wa kumbukumbu, kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali, wenye ujuzi wa kompyuta.

b) Kazi na majukumu

- kuorodhesha barua zinazolingia masjala kwenye rejista (incoming correspondence register)
- kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi kwenye rejista (outgoing Correspondence register)
- kusambaza majalada kwa watendaji (action officers)
- kupokea majalada yanayorudi masjala toka kwa watendaji
- kurudisha majalada kwenye shubaka / kabati la majalada (racksfiling cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa
- kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (File Tracking)


2. MAELEKEZO

- i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania wasiozidi umri zaidi ya miaka 45 na wasiopungua umri wa miaka 18.
- ii. Waombaji wote lazima waambatanishe wasifu binafsi (CV) zenye wadhamini wawili na mawasiliano ya uhakika, anuani, barua pepe na namba za simu.
- iii. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya TANGAZO LA KAZI,
- iv. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
 - a) Stashahada/Cheti cha utaalumu kulingana na sifa za nafasi husika.
 - b) Cheti cha mtihani wa kidato cha nne na cha sita.
 - c) Cheti cha kuzaliwa.
 - d) Picha mbili za passport size.
- v. Hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (Result slip) na "Transcript" hazitafanyiwa kazi.
- vi. Watumishi wa Umma walioajiriwa wapitishe maombi yao kwa waajiri wao.
- vii. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na cheti cha Taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la mtihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya ufundi la Taifa (NACTE).
- viii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au kingereza.
- ix. Watakaotwa kwenye usaili watajigharamia wenyewe.
- x. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe **16/08/2023** saa **9:30** alasiri, baada ya tarehe hiyo kupita maombi hayatapokelewa na watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri www.njombedc.go.tz na kwenye mbao za matangazo za Halmashauri.

Barua zote zitumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE,
S.L.P 547,
NJOMBE.

Tangazo hili limetolewa na:-


Christopher A. Sanga
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NJOMBE